



MAASAI MARA UNIVERSITY

REGULAR UNIVERSITY EXAMINATIONS 2018/2019 ACADEMIC YEAR

SCHOOL OF EDUCATION BACHELOR OF EDUCATION

COURSE CODE: CIM 316
**COURSE TITLE: SPECIAL METHODS IN
KISWAHILI**

DATE: 26/04/2019

TIME: 1430 - 1630 HRS

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

Question **ONE** is compulsory

Answer any other **TWO** questions

- 1 (a) Eleza namna sifa za lugha zinavyoweza kumsaidia mwalimu kufundisha vipengele mbalimbali vya Lugha. **(Alama 5)**
- b) Eleza nafasi ya Kamusi katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili. **(Alama 5)**
- c) Andika lengo la somo linalojikita katika kila mojawapo wa viwango vya maarifa vifuatavyo :
 i. Ufahamu
 ii. Uchanganuzi
 iii. Usanisi **(Alama 6)**
- d) Eleza umuhimu wa shughuli za wanafunzi katika andalio la funzo. **(Alama 4)**
- e) 'Ufahamu wa kusikiliza na kusoma huwa katika viwango tofauti ambavyo ni muhimu kwa mwalimu kuzingatia.' Jadili viwango hivyo. **(Alama 10)**
2. a. Kwa kutoa mifano mwafaka, eleza namna unavyoweza kuwasaidia wanafunzi wako kutambua maudhui katika matini za fasihi. **(Alama 10)**
- b. Fafanua mambo yoyote matano yanayozingatiwa wakati wa kuteua mada za somo katika silabasi. **(Alama 10)**
3. a) Huko ukitoa mifano, eleza namna unavyoweza kutumia nadharia ya utabia kufundisha sarufi. **(Alama 10)**
- leza udhaifu unaoweza kukabiliana nao unapofundisha Kiswahili kwa misingi ya nadharia ya utabia. **(Alama 10)**
4. Eleza mchango wa tume zifuatazo kwa lugha ya Kiswahili. **(Alama 20)**
- i. Tume ya Ominde (1964)
 ii. Tume ya Gachathi (1976)
 iii. Tume ya Mackey (1981)
 iv. Tume ya Koech (1999)
5. (a) Eleza manufaa ya kufundisha sarufi bila kutanguliza kanuni zake. **(Alama 10)**
- b) Fafanua hatua zozote tano unazoweza kutumia katika kufundisha ushairi wa Kiswahili. **(Alama 10)**

.....MWISHO.....